GREDI YA TISA - MWAKA 2026

KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

Muda: Saa 1 dakika 40

Jina la Mtahiniwa	**Nambari ya Mtahiniwa**
Jina ya Shule Yako	**Nambari ya Shule**
Sahihi ya Mtahiniwa	**Tarehe**

902/1

Karatasi ya 1

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 6.

Neema alikuwa akirejea nyumbani kutoka maktaba majira ya saa kumi na mbili jioni. Mji ulikuwa umejaa pilikapilika za magari na watu waliokuwa **wakikimbizana kama kuku waliotupwa mawe**. Alikuwa amebeba mkoba mzito uliojaa vitabu na tarakilishi yake ya zamani aliyopewa na shangazi yake kama zawadi ya kujiunga na chuo kikuu.

Alipokuwa akivuka barabara karibu na soko la Marikiti, macho yake yaliangukia bahasha ya kahawia iliyokuwa imetupwa kando ya jaa. Ilikuwa nene na ilionekana kuwa na kitu ndani. Moyo wake ulidunda kwa nguvu. Akaichukua kwa tahadhari na kuifungua kidogo. Ndani kulikuwa na marundo ya pesa, na karatasi ndogo iliyoandikwa "Ada ya upasuaji wa mama".

Neema alihisi damu ikimkimbia mwilini. "Ala! Pesa hizi ni za nani? Zinaonekana ni za mtu aliyekuwa na shida kubwa!" Aliwaza huku akiangaza macho yake kila upande. Kando yake, aliona kijana mmoja aliyevalia kofia nyeusi akimkazia macho kwa jicho la pembeni. Kijana huyo **alikuwa amesimama kama bendera ya chama** katikati ya kundi la watu, lakini macho yake yalikuwa kwenye bahasha hiyo.

Neema alichanganyikiwa. Akili yake ilimwambia atoweke haraka na pesa hizo kwani karo yake ya chuo ilikuwa imechelewa miezi mitatu na alikuwa karibu kufukuzwa. Lakini dhamiri yake ilimwambia kinyume. Alikumbuka maneno ya bibi yake: "Mkono mtupu haulambwi, lakini mali ya dhuluma haidumu. Heshima na uaminifu ni taji la mwanadamu."

Kabla hajafanya uamuzi, aliona mzee mmoja akilia huku akijishika kichwa karibu na mahali alipoipata bahasha. Mzee alikuwa akimuuliza kila mtu "Mmeona bahasha yangu ya kahawia?". Neema aligundua bila shaka kuwa pesa hizo ni za mzee huyo. Bila kusita, licha ya kijana wa kofia kumtisha kwa macho, alimsogelea mzee na kumpatia bahasha yake.

Mzee alifurahi kupita kiasi na kumwombea mema. "Mungu akubariki mwanangu. Umenionyesha kuwa bado kuna watu wenye utu katika mji huu uliojaa mbweha."

1. Mwandishi ametumia kauli **"wakikimbizana kama kuku waliotupwa mawe"** kuonyesha nini?
A. Harakati na fujo nyingi za watu mjini.
B. Watu wa mjini wanapenda kufuga kuku.
C. Watu wa mjini ni waoga kama kuku.
D. Kuku wengi hutembea mjini wakati wa jioni.

2. Kwa nini Neema alipatwa na mshtuko mkubwa baada ya kuona pesa?
A. Kwa sababu alikuwa ameiba pesa hizo.
B. Kwa sababu pesa hizo zilikuwa nyingi na zilihusiana na maisha ya mtu
C. Kwa sababu kijana wa kofia alikuwa anamfuata.
D. Kwa sababu alikuwa amepoteza karo yake ya shule.

3. Kauli **"alikuwa amesimama kama bendera ya chama"** ina maana gani katika muktadha huu?
A. Kijana alikuwa maarufu sana.
B. Kijana alikuwa amevaa nguo zenye rangi nyingi.
C. Kijana alikuwa mwanachama wa chama cha siasa.
D. Kijana alikuwa amesimama waziwazi na kujionyesha bila haya akingojea fursa ya kudhuru.

4. Mgogoro wa ndani wa Neema ulitokana na nini?
A. Kutotaka kurejea nyumbani.
B. Mvutano wa fikra kati ya haja yake binafsi ya karo na maadili yake ya uaminifu.
C. Kuogopa kijana wa kofia nyeusi.
D. Kutokujua hesabu ya pesa zilizokuwa kwenye bahasha.

5. Methali **"Mkono mtupu haulambwi"** kama ilivyotumika hapa, inadhihirisha nini?
A. Lazima mtu afanye kazi ili apate kitu.
B. Ni sawa kuchukua pesa za mtu mwingine kama una njaa.
C. Neema alikuwa akijitetea kuchukua pesa kwa sababu ya umaskini wake.
D. Bibi yake alimfundisha kuomba